

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**WILAYA YA WANGING'OMBE.**



Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,  
287 Barabara ya Halmashauri,  
S.L.P 624,  
**59381 WANGING'OMBE NJOMBE.**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb Na: DC/WANG/D.5/01/35**

**30/08/2023.**

Kwa Wananchi wote,

**WILAYA YA WANGING'OMBE.**

Yah: **TANGAZO LA UANDIKISHAJI WA VIJANA WA KUJIUNGA NA JESHI LA**  
**KUJENGA TAIFA KWA UTARATIBU WA KUJITOLEA (HIARI) MWAKA 2023/2024**

**1.0 UTANGULIZI**

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Wanging'ombe inapenda kuwatangazia vijana wote wanaopenda kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa utaratibu wa kujitolea kwa muda wa miaka miwili kwa mwaka 2023/2024.

**2.0 WAOMBAJI WANATAKIWA KUWA NA SIFA ZIFUATAZO:**

1. Awe raia wa Tanzania.

**2. Umri:**

- a) Kwa vijana wenye elimu ya Darasa la Saba umri ni kuanzia miaka **16** hadi **18**, waliomaliza Elimu ya Msingi Kuanzia Mwaka **2020, 2021, 2022** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Msingi.
- b) Vijana wenye elimu ya Kidato cha Nne umri usiwe zaidi ya miaka **20**, waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia Mwaka **2020, 2021, 2022** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate). Awe na

ufaulu wa Daraja la Kwanza hadi Daraja la Nne. Kijana mwenye Daraja la nne awe na ufaulu wa alama kuanzia 26 hadi 32.

- c) Vijana wenye elimu ya Kidato cha Sita umri usiwe zaidi ya miaka 22, waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia Mwaka 2020, 2021, 2022 na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya sekondari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate). Awe na ufalu wa Kuanzia Daraja la Kwanza hadi Daraja la Nne.
  - d) Vijana wenye elimu ya Stashahada umri usiwe zaidi ya miaka 25, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.
  - e) Vijana wenye Elimu ya Shahada umri usiwe zaidi ya miaka 26 awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha chuo.
  - f) Vijana wenye Elimu ya Shahada ya Uzamili umri usiwe zaidi ya miaka 30, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.
3. Awe na afya njema, akili timamu na asiwe na alama yoyote ya michoro mwilini (Tattoo).
  4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.
  5. Awe na Kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
  6. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate).
  7. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo wala kuajiriwa na idara nyingine Serikalini.
  8. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma kwa kundi la kujitolea na kundi la lazima (Mujibu wa Sheria).
  9. Asiwe amejihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana nayo.

10. **Angalizo:** Kijana atakayepatikana na nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua kali za kisheria kulingana na taratibu zilizopo.

**3.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

- i. Barua za maombi zitaanza kupokelewa kuanzia tarehe **30 Agosti, 2023** hadi tarehe **05 Septemba, 2023** saa **9:30 Alasiri**.
- ii. Barua zote za maombi zipitishwe na Watendaji wa vijiji
- iii. Kila Mwombaji abandike picha yake ya passport size kwenye barua yake ya maombi.
- iv. Barua zote za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Wanging'ombe,  
287 Barabara ya Halmashauri,  
S.L.P 624,  
**59381 WANGING'OMBE NJOMBE.**



Veronica Gerald  
KATIBU TAWALA WILAYA  
WANGING'OMBE

